**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA**
**TUMAINI SHULE YA SEKONDARI**

S.L.P.533,
IRAMBA-SINGIDA
**31/03/2022**

**Mkuu wa shule: Zainabu I. Mtinda**
**Simu: 0755278326/0787723373/0716723373**
**Barua pepe: tumainisecondary1969@gmail.com**
**Blog: tumainisecondary.blogsport.com**
**Instagram: tumainisecondaryschool**

**Makamu mkuu wa shule**
**0752607620/ 0787160394/0769184185**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………SLP…………………..

**YAH:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI **TUMAINI** HALMASHAURI YA WILAYA YA **IRAMBA** MKOA WA **SINGIDA**.MWAKA **2022**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari T**umaini** iliyoko Wilaya ya **IRAMBA** katika mkoa wa **SINGIDA** mwaka **2022** tahasusi ya HGE/HGL/HGK/HKL/ **KARIBU SANA TUMAINI SHULE YA SEKONDARI**

Shule iko kilomita 70 kutoka Singida mjini.

Kama utapanda basi la moja kwa moja toka Dar es salaam, Moshi, Arusha N.K yaani mabasi yote yenye uelekeo wa kwenda Mwanza, shinyanga (barabara ya kati) atashuka kituo kinachoitwa KITUSHA, na hapo atapanda bodaboda au gari ndogo aina ya HIACE, ni umbali wa kilomita 8 mpaka shuleni..

Kutoka Singinda mjini atapanda mabasi katika kituo cha mabasi msufini na jengo CCM, hapo utakuta magari aina ya **HIACE** ambayo huondoka Singida kati ya saa 6:30 na saa 7:00 mchana kila siku kwenda Kinampanda mahali shule ilipo. Nauli ni shilingi 4,000/= endapo atachelewa muda huo apande gari yeyote inayoenda kiomboi au Igunga katika vituo hivyo vya magari.na ashuke kituo cha magari KITUSHA. Endapo mwanao atapanda mabasi ya kutoka Tabora, Nzega, Kahama, au Mwanza kwenda Arusha au Dar es salaam ashukie sehemu iitwayo **KITUSHA**.

Kutoka Kitusha kuna umbali wa kilomita nane (8) mpaka shuleni hivyo atakodisha pikipiki mpaka shuleni au atasubiri maabasi aina ya HIACE yatokayo Singida Mjini kufika shuleni.

Muhula wa masomo unaanza kwa kadri ya maelekezo ya Wizara inayoshughulikia masuala ya Elimu Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti mara tu tarehe tajwa itakapotangazwa.

**muda wa kuripoti ni mchana kuanzia saa saba kamili mchana hadi saa kumi na moja na nusu jioni.**

Ninasisitiza mwanafunzi awahi shule kwa muda na tarehe iliyotangazwa

Scanned with CamScanner

## 2. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare ya sahule

a) Sare ya shule ni sketi bluu Bahari (light blue)-sketi 2 kitambaa kizito cha suti grade 1 mshono wa Rinda bapa(box)mbele na nyuma, sketi iwe ndefu mpaka chini (juu kidigo ya viatu) Mashati mawili(2) ya mikono mirefu.

b) Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe nyeupe na ndefu kufika usawa wa nyonga, na hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya halua. (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine)

c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi-Jozi mbili(2)

d) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta na T-shirt rangi ya bluu,raba rangi yoyote(jozi moja) na track suit rangi ya kijivu(jozi moja)

e) Soksi nyeupe jozi tatu.

f) Sweta bluu Bahari yenye shepu ya **V** mbele.

g) Nguo za kushindia(shamba dress) sketi nyeusi mbili,mshono marinda ya kutazamana.

h) T-shirt mbili(2) za kuvaa nje ya darasa( aje na shilingi 20,000/=)

i) Nguo za nyumbani haziruhusiwi isipokuwa aje na kanga/vitenge pair moja tu atatumia wakati wa kuoga.

### 2.2 Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni, mwanafunzi anatakiwa kulipa shilingi 35,000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na.**50601100179(Tumaini secondary school Recurrent A/C) NMB** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Bank pay in slip) aje nayo anaporipoti shule.

**b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi.**

i. Shilingi 15,000/=kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/=kwa ajili ya kitambulisho
iii. Shilingi 20,000/=kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/=kwa ajili ya kuwalipa wapishi na walinzi na vibarua wengine
v. Shilingi 2,000/=nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza pamoja na Bima ya Afya.
vii. shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock
viii. shilingi 5,000/=fedha ya tahadhari (haitarejeshwa)

**NB:** fedha zote zilipwe kwenye akaunnti ya shule **50601100179 (tumaini secondary school Reurrent A/C) NMB** shule haipokei mchango wowote wa taslimu. Mwanafunzi aje na paying slip mbili (moja paying slip ya ada na nyingine ya michango)

Scanned with CamScanner

**2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

**2.3.1.Vifaa vya darasani**

(a)Madaftari makubwa 8(counter book) (b) Kalamu za wino (c) Mathematical set

(d)Ream A4 moja (01) ya karatasi kwa ajili ya mitihani (e) Penseli (f) Rula

(g) Dictionary advanced learner

(h) Calculator-non programmable kwa Geography, economics na sayansi

(j) Aje na results slip (original),picha nne passport size za wazazi au walezi wanaoweza kukutembelea shuleni.

(k)Aje na vitabu kulingana na masomo yake kwa ajili ya kujifunzia

**2.3.2.Vifaa vya kulalia**

(a)Godoro (sponji) futi 2.5 inch 4 (b)Net ya Mbu

(c)Mashuka mawili(2) light blue (e) Mto wenye foronya light blue (f)Blanketi 1

2.3.3.**Vifaa vya chakula**

(a)Sahani (b) Bakuli (c) kijiko (d) kikombe (e) Galoni ya kuwekea maji ya kunywa

2.3.4.**Vifaa vya usafi binafsi**

(a)Ndoo 2( lita 20 na lita 10) (b)Mswaki na dawa ya meno (c) Malapa (d)Sabuni za kufulia na kuogea. Na mahitaji ya kike (nguo za ndani na taulo za kike)

**VIFAA VYA USAFI:**

(e)**HKL na PBC**-waje na jembe lenye mpini,**HGK** na **HGE** waje na Reki yenye mpini na **HGL** -Panga lililonolewa

**NB: Mifagio ya ndani ( soft broom) na dawa ya chooni (ARO)**

**mifagio ya kudekia (rubber broom) na mifagio ya chelewa ni kwa wote.**

Wako katika ujenzi wa Taifa.

**Z.I.MTINDA**

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI TUMAINI
S.L.P. 555-KINAMPANDA

Scanned with CamScanner

# SHULE YA SEKONDARI TUMAINI.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

i. Utoro
ii. Wizi
iii. Uasherati, ushoga na ulawiti , Kuoa au kuolewa.
iv. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
v. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya .
vi. Uvutaji wa sigara au bangi.
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
viii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
ix. Kudharau Bendera ya Taifa
x. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xii. Kugoma kwa namna yoyote au kuchochea vurugu
xiii. Kutoa lugha ya matusi au lugha chafu kwa mwanafunzi,walimu,walezi,na jamii kwa ujumla.
xiv. Kumdharau mwalimu, Kiongozi, Mfanyakazi na jamii kwa ujumla
xv. Kutohudhuria vipindi kwa uzembe
xvi. Kutofanya mitihani kwa makusudi/bila sababu ya msingi
xvii. Kushirki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xix. Kumiliki simu.

Scanned with CamScanner

**FOMU A:**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI TUMAINI.**

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA MWANAFUNZI

A. **Habari za mwanafunzi**:

| Picha Ya mwanafunzi |
|---|

i. Jina kamili…………………………………………………………………………………

ii. Tarehe ya kuzaliwa……………………….Wilaya………………………….

iii. Dini……………………….Dhehebu…………………………………………….

**Mahali atakapokuwa anaenda likizoni:**

i. Jina……………………………Uhusianao……………..Mahali……………..

ii. Jina……………………………Uhusiano……………..Mahali……………..

**Kukubali nafasi:**

Mimi…………………………………………nimeona maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Tumaini. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutii sheria za shule. Nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na kuchapa kazi za mikono kwa bidii ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake.

**Saini………………………..Tarehe………………………………………………………….**

**B. Habari za Mzazi/Mlezi**

| Picha Ya Mzazi/mlezi |
|---|

i. Jina kamili…………………………………………………………………………

ii. Yeye ni mzazi au mlezi………………………………………………………

iii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi…………………………………………

iv. Kazi yake……………………………………………………………………………

v. Anwani ya kazini…………………………………………………………………

vi. Namba ya simu……………………………………………………………………

vii. Anwani ya nyumbani……………………………………………………………………

viii. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:

Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wnagu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondari Tumaini.

**Jina…**…………………………………….**Saini……………………Tarehe**……………..

Scanned with CamScanner

FORM B:

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A:

**TO**: The Medical Officer
________________________
________________________
________________________

**FROM**: The Headmistress,
Tumaini Sec. School,
P.O. Box 533,
Kinampanda,
IRAMBA – SINGIDA.
DATE______________

NAME__________________________________

Please examine the above named person as to her fitness for re-engagement as a student in our school.

Signature __________________________

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above named person ad consider that she is____________
__________________________________________________________________
__________________________________________________________________

Date________________________ Signature ___________________________

Station______________________ Designation _________________________

Scanned with CamScanner